**Learning by Ear – Climate Change**

**Episode 02**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- LORNA (16)
- MRS KIMAU – SCIENCE TEACHER & LORNA'S MOTHER (45)

Scene 2:

- ALEX (15)
- MR LANSARD – ALEX'S FATHER AND MEMBER OF PARLIAMENT FOR DHOWVILLE (45)
- MR KAPOOR – MANAGING DIRECTOR AND OWNER OF THE NATIONAL POWER BOARD (60)

**Intro:**

Kwa mara nyingine karibu msikilizaji katika mfululizo wa mchezo huu wa Radio “Noa Bongo Jenga Maisha Yako” tukiwa bado tunaendelea na hadithi yetu kuhusu mabadiliko ya hali ya Hewa. Katika makala haya,Carol na Lorna wagundua njama ya ujenzi wa kiwanda cha umeme kinachotiliwa pono na vyombo vya habari kama ni mradi utakao weza kutatua tatizo la ukosefu wa umeme katika eneo lao.Hata hivyo wasichana hawa wanashuku kuwa huenda mradi huu ukawa na athari kubwa kwa mazingira sio tu katika kijiji chao bali taifa zima kwa jumla. Kwa mengi zaidi endelea kuwa nasi hadi mwisho wa kipindi.

**Scene One: in the kitchen at Lorna’s house**

**SFX ATMO:** **KITCHEN SOUNDS – COOKING, RADIO, OPENING CLOSING OF CUPBOARDS**

**1. LORNA:** Mama, unadhani tunapaswa kuwa na hofu kuhusu mapendekezo ya ujenzi wa kiwanda cha umeme ambao tumekuwa tukiuzungumzia leo darasani.?

**2. MRS KIMAU:** Eeeh, ndio, mimi binafsi nina wasi wasi, kwani kwa kuzingatia yaliyoandikwa magazetini, kiwanda hiki ndicho kitakachokuwa kikubwa zaidi hapa nchini. Unajua Afrika ni mojawapo ya maeneo yaliyoathirika zaidi na mabadiliko ya hali ya hewa.

**3. LORNA:** Kila mara mimi husoma kuhusu suala la hili la mabadiliko ya hali ya hewa, lakini bado sielewi vipi linavyotuathiri hapa Afrika..

**SFX:** **PUTTING MEAT ON THE GAS TO FRY**

**4. MRS KIMAU:** Ili kukutoa taka masikioni, kila bara na nchi ina misimu yake ya hali ya hewa, au tusema ripoti ya utabiri wa hali ya hewa..

**5. LORNA:** Na yetu ni ipi?

**6. MRS KIMAU:** Kimsingi sisi hapa tumekuwa kila mara na misimu miwili ya mvua,- mvua za masika ambazo huanza mwezi wa Aprili hadi Mei, kisha mvua za Vuli ambazo huja mwezi Novemba. Halafu tumekuwa na msimu wa kiangazi ambao huanzia mwezi Disemba hadi mwezi Machi. Kwa kawaida msimu wa baridi huanza mwezi Julai hadi Septemba.

**7. LORNA:** Lakini hali hiyo sasa imebadilika!. Sasa tuko mwezi Januari, na jana ililinyesha mvua kubwa isiyo ya kawaida.

**8. MRS KIMAU:** Ni kweli, Lorna! Hayo ndiyo ninayo maanisha ninapozungumzia mienendo ya hali ya hewa. Wakati nilipokuwa mdogo, misimu hii ilikuwa inajulikana bayana kabisa. Ungeweza kutabiri lini utaanza msimu wa mvua za masika-tungejitokeza barabarani kufurahia mvua hizo za masika. Wakulima nao wangesherehekea kuanza kwa msimu huo baada ya kuandaa mashamba yao.

**9. LORNA:** Sasa kwa nini hali hiyo imebadilika sasa?

**10. MRS KIMAU:** Ehh….hali hii ndiyo watalaam wanayoiita global warming yaani ongezeko la ujoto dniani. Wakati kiwango cha joto ardhini na baharini kinapoongezeka, na hivyo kusababisha mabadiliko kwenye mikondo ya misimu ya hali ya hewa.

**11. LORNA:** Na nadhani hii pia inahusiana na athari za gesi chafu inayotoka viwandani ambayo tulijifunza leo darasani.

**12. MRS KIMAU:** Hiyo ni kweli. Kumekuwa na ripoti kadhaa za jopo la kimataifa la mabadiliko ya hali ya hewa, kundi lililoundwa na serikali mbalimbali na Umoja wa Mataifa ili kutathmini kiwango cha mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababishwa na binadamu.

**13. LORNA:** Ni maazimio yapi waliyoyafikia?

**14. MRS KIMAU:** Kitu muhimu walichogundua ni kuwa kiwango cha joto ulimwenguni kinazidi kuongezeka hasa kutokana na shughuli za binadamu. Hii labda inatokana na ujenzi wa viwanda visivyozingatia usafi wa mazingira na pia uchafuzi unaotokana na uendeshaji magari kila mahali. Nishati zinazotumika kama vile Diesel au petroli hutoa dioksidi ya Kaboni ambayo huchangia uchafuzi wa mazingira

**15. LORNA:** Kwa hivyo huenda hiyo ndio sababu kuna joto zaidi na tunalazimika kulala tukiwa tumewasha. Mimi sikumbuki nikilala na feni nilipokuwa mdogo!

**16. MRS KIMAU:** Wakati huo hungehitaji kutumia feni . Lakini siku hizi joto limeongezeka sana. Inaonekana tuna vipindi virefu vya ukame bila mvua! Na kisha kwa ghafla mvua kubwa hunyesha hasa katika maeneo ya kaskazini mwa nchi inayosababisha mafuriko.

**17. LORNA:** Nakumbuka kuona picha za mafuriko kwenye televisheni. Magari madogo yalikuwa yakielea na watu na hata nyumba zilisombwa na mafuriko hayo.

**18. MRS KIMAU:** Watabiri wa hali ya hewa, wanasayansi na hata babu yako ambaye amekuwa akijigamba kwamba anaweza kutabiri ni lini mvua zitakaponyesha, yaonekana ameshindwa kabisa kutabiri hali hiyo kwa sasa!. Kwa hivyo watu barani Afrika wanaotegemea ardhi, bahari na hali nzuri ya hewa kwa shughuli zao, mambo yameanza kuwabadilikia na kuwa magumu zaidi..

**SFX:** **SOUND OF FAT FRYING GETS LOUDER**

**19. LORNA:** Ohh Mama, nadhani umemuunguza huyo samaki!

**20. MRS KIMAU:** Aagh! Hata sikuwa na umakini!. Mimi huudhika kuhusu mazingira hasa kwa nyie vijana..

**21. LORNA:** Naelewa hilo.

**22. MRS KIMAU:** Lakini kuna jambo moja, Lorna. Kuna watu wengi wenye nadharia kwamba kupanda kwa kiwango cha joto, kiwango cha maji baharini na mabadiliko ya hali ya hewa ni jambo la kawaida tu! Na bila shaka hata wanasayansi hawawezi kuwa sawa asilimia mia moja kwa mia.

**23. LORNA:** Akiwa darasani Alex huwa hivyo tu! Angalau amekuwa hivyo hadi leo. Lakini nafikiri kwa sehemu inatokana na babake. Si unajua babake ni mwanasiasa! Ni mwanasiasa na inaonekana anahusika katika mradi wa ujenzi wa kiwanda cha umeme hapa mjini.

**24. MRS KIMAU:** Kweli? Basi ni lazima umsaidie aweze kuelewa. Labda itakuwa muhimu kwetu katika kumshawishi Babake. Tafuta ujue kwa hakika ni nani wanaohusika na uwawajibishe watoe majibu kamili. Chunguza iwapo kweli wanazingatia na kujali usafi wa mazingira.

**25. LORNA:** Hilo ni wazi zuri! Labda tunaweza kuanzisha kundi fulani kushinikiza kundi fulani ili kusimamisha kiwanda hiki cha umeme? Lakini mama tunaweza kula sasa? nahisi njaa!

**26. MRS KIMAU:** Mimi pia!

**SFX:** **SOUND OF PLATES, CUTLERY CLINKING**

**Scene Two: Proposed site for thermal power station**

**SFX ATMO:** **SEA SOUNDS, WAVES**

**27. MR LANSARD:** Ehe Alex,hapa ndipo mahali palipopendekezwa ujenzi wa kiwanda cha umeme tunachozungumzia kila siku.Bado mradi wenyewe haujaanza, lakini katika muda wa miezi michache ijayo, baada ya kupata kibali, bila shaka utaona shughuli zikiongezeka hapa.

**28. ALEX:** Lakini Baba, hii ni moja wapo ya sehemu za kuvutia katika ufuo huu wa bahari!.Mara nyingi sisi huja kucheza kandanda pale ufuoni.

**29. MR LANSARD:** Alex, lakini kunazo sehemu nyingi tu za ufuo katika eneo la kusini. Na mbali na hayo, hudhani ni muhimu kuwa na umeme kuliko ufuo wa kuchezea?

**30. ALEX:** Na je kuhusu uchafu utakaotoka kiwandani? Machujo ya mafuta hutoa kiasi kikubwa cha taka zenye sumu. Una hakika uchafu huu hautamwagwa baharini? Na je sisi pia hatutalazimika kuvuta hewa iliyochafuliwa na sumu hiyo?

**SFX:** **FOOTSTEPS APPROACHING ON THE GRAVEL**

**31. MR KAPOOR:** Habari za mchana mabwana! Habari gani bwana Lansard? Nafurahi kukuona ukikagua eneo la ujenzi .Huyu kijana ni nani?

**32. Mr LANSARD:** Ahh, habari za mchana bwana Kapoor. Huyu ni kijana wangu mdogo anaitwa Alex. Anapenda kunisaidia kutangaza kiwanda chako cha umeme, kwa hivyo ninamtembeza hapa!

**33. MR KAPOOR:** Sawa kabisa, hilo ni jambo la busara. Si itakua vyema mwaka ujao wakati kama huu wakati kila mkaazi wa mji huu atapata umeme kwa saa 24 bila ya kukatizwa mara kwa mara, kutazama televisheni wakati wote, na pia taa ya kufanyia kazi zako za nyumbani!. Uwezekano usio na mwisho!

**36. ALEX:** Ndio bwana lakini wanafunzi wengi wa darasa langu shuleni wana wasiwasi kwamba huenda mradi huo utaharibu mazingira. Yaani ni maana tumekuwa tukijifunza kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na..

**37. MR LANSARD:** Na hayo yote yanapendeza sana Alex! Lakini Bw Kapoor ni mtu wa shughuli nyingi na hana muda wa kusikiliza kuhusu masomo yako. **(now talking to Mr Kapoor)** Samahani kwa kusumbuliwa na kijana wangu. Si unajua vijana walivyo wanapokuwa wadogo!

**40. ALEX:** Sipingi ujenzi wa kiwanda hiki ,lakini napendekeza kiwanda kinachozingatia usafi wa mazingira badala ya kile kitakachotumia machujo au mabaki ya mafuta na Diesel.
Na kwanini kusijengwe kiwanda kinachotumia umeme unatokana na maji au upepe? Kuna upepe mwingi sana unaotoka baharini.

**43. MR KAPOOR:** Bwana Lansard, labda mwanao hafai kutusaidia kutangaza kiwanda hiki. Nafikiri bora utumie nafasi yako kama mbunge wa eneo hili la Dhowville kuwashinikiza kidogo wananchi kutoa msukumo zaidi wa ujenzi wa kiwanda hiki. Mradi huu utagharimu pesa nyingi sana! Na iwapo kila kitu kitaenda kama ilivyopangwa basi bila shaka utapata bakshishi yako..

**48. MR LANSARD:** Sidhani kama kutakuwa na matatizo yoyote bwana Kapoor.

**49. MR KAPOOR:** Vyema! Hilo ndilo ninalotaka kusikia. Sasa nalazimika kwenda kwenye mkutano wangu na bodi ya wawekezaji.

**SFX:** **CAR STARTING AND DRIVING OFF ON GRAVEL**

**51. MR LANSARD:** Alex, kwa nini unamzungumza namna hiyo na mtu muhimu kama yule?

**52. ALEX:** Samahani Baba, lakini nadhani anasema uongo kuhusu suala la uharibifu wa mazingira. Kwani wewe hujali tena mazingira yetu?

**53. MR LANSARD:** Hiyo inatosha Alex! Sasa nitakufungia kwa muda wa mwezi mmoja, ingia ndani ya gari twende nyumbani haraka!

**SFX:** **OPENING, CLOSING CAR DOOR AND DRIVING OFF**

**END OF EPISODE TWO**

**Outro:**

Na hadi kufikia hapo ndipo tunafika mwisho wa kipindi cha leo cha Noa Bongo Jenga Maisha yako. Mchezo ulioandikwa na Victoria Averill.

Ungana nasi wakati mwengine kwa usikie jinsi Joshua anavyoshuhudia mabadiliko ya hali ya hewa yanavyoathiri maisha ya Babake, na pia iwapo Joshua atajiunga na wenzake shuleni. Iwapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe . Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa.